**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO**

# BARAZA LA MICHEZO LA TAIFA (BMT)

**24 Desemba, 2025**

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

## UCHAGUZI WA VIONGOZI WA KAMATI YA PARALIMPIKI TANZANIA (TPC)

Baraza la Michezo la Taifa (BMT) linapenda kuwataarifu wanachama na wadau wa michezo ya Palalimpiki Tanzania (Michezo ya Watu wenye Ulemavu wa Viungo), kuwa Uchaguzi wa Viongozi wa Kamati ya Paralimpiki Tanzania unatarajiwa kufanyika tarehe 25 Januari, 2026, Jijini Dar es Salaam.

Fomu za kugombea nafasi tofauti katika uchaguzi huo zitaanza kutolewa katika Ofisi za BMT zilizopo Uwanja wa Benjamin Mkapa tarehe 24 Desemba, 2025 hadi Januari 21, 2026 na zinapatikana katika tovuti ya Baraza ambayo ni www.bmt.go.tz

Aidha, Usaili wa wagombea wa nafasi hizo unatarajiwa kufanyika tarehe 24 Januari, 2026 katika Ofisi za Baraza la Michezo la Taifa, Jijini Dar es salaam.

Nafasi zinazogombewa katika uchaguzi huo ni pamoja na:

| Nafasi | Ada |
|---|---|
| 1. Rais<br>2. Makamu wa Rais<br>3. Katibu Mkuu<br>4. Katibu Mkuu Msaidizi<br>5. Mweka hazina | 70,000/= |
| 6. Mwakilishi wa Wanawake<br>7. Mwakilishi wa Wachezaji<br>8. Mjumbe wa Kamati ya Utendaji | 30,000/= |

**Sifa za wagombea**

- **i.** Awe Raia wa Tanzania
- **ii.** Awe na Elimu isiyopungua Kidato cha Nne (Cheti cha Elimu ya Sekondari)

Uwanja wa Benjamin Mkapa, (Ghorofa ya pili), Barabara ya Taifa, S.L.P 20116, **DAR ES SALAAM.**
**Simu:** +255 (734 220 164 info@nationalsportscouncil.go.tz na **Tovuti**:www.bmt.go.tz

- **iii.** Awe na ujuzi na uzoefu wa katika Uongozi wa Vyama vya Michezo Shiriki vya TPC
- **iv.** Awe na umri usiopungua miaka ishirini na tano (25)
- **v.** Awe hajawahi kupatikana na hatia yoyote ya makosa ya jinai.

Malipo ya fomu yafanyike katika Akaunti ya Baraza, kwa kutumia mfumo mpya wa malipo ya Serikalini.

Ili kupata namba ya malipo (Control Number) mgombea anashauriwa kupiga namba ya simu ifuatayo; 0683 578 186

Aidha, fomu ya kugombea iwasilishwe Baraza ikiambatishwa na risiti ya malipo pamoja na nakala za nyaraka kulingana na sifa mahususi zilizoainishwa katika katiba ya Kamati ya Paralimpiki Tanzania.

BMT inatoa wito kwa yeyote mwenye sifa kwa mujibu wa Katiba ya Kamati ya Paralimpiki Tanzania kujitokeza kuchukua fomu kwa ajili ya uchaguzi huo na maendeleo ya Mchezo huo nchini.

**Imetolewa na**

**Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano**

**BARAZA LA MICHEZO LA TAIFA (BMT)**